



**Weka kijikaratasi hiki salama**  
Ikiwa unahitaji maelezo haya



**Public Health**  
Northamptonshire

# VIRUSI VYA CORONA

Taarifa muhimu kwa wakaaji

**Kesi za COVID-19 (virusi vya corona) zazidi kuongezeka katika eneo hili nawe pamoja na jamii yako muko hatarini.**

**Tunahitaji kufanya kazi pamoja ili kuzuia kufungwa kwa mtaa wetu. Hatuna budi kufuata masharti yafuatayo:**

- Punguza uwezavyo kujumwika na jamii
- Ikiwa itabidi utoke nje, kaa umbali wa mita mbili kando na mtu mwingine
- Tumia barakoa ili kufinika uso ukiwa madukani unapokua chini ya mita mbili kutoka kwa mtu mwingine
- Nawa mikono yako itakate vizuri kabisa kila mara kwa sekunde 20 kila zamu
- Iwapo una dalili za virusi vya corona, tafadhali fuata mwongozo uliyo nyuma ya kijikaratasi hichi

**#NorthantsTogether**

## COVID-19 Dalili zifuatayo huonekana:

- Joto kali mwilini
- Kukohoa kupya mfululizo
- Kupoteza au badiliko la hisia zako za harufu au ladha

## Ikiwa una dalili za COVID-19:

- Usiende kazini. Fanya kazi nyumbani mwako, au upige ripoti kuwa umgonjwa, jitenge mwenyewe na uitishe kupimwa
- Kaa nyumbani, jitenge na upate kupimwa
- Hata kama una kiasi kidogo cha dalili za COVID-19, pata kupimwa
- Ikiwa wahudumiaji wa NHS, Idara ya Kupima na mfuatilio wakiwasiliana na wewe, na wakushauri ujitenge, kaa nyumbani kwa siku 14

## Ili kupimwa, fanya limoja:

- Jiandikishe kwa mtandao wa **nhs.uk/coronavirus**
- Piga simu **119**
- Vifaa vya upimaji nyumbani vyaweza kuagizwa, ikiwa vipo



Kwa ushahuri zaidi wa hivi majuzi  
zuru [www.northamptonshire.gov.uk](http://www.northamptonshire.gov.uk)

Kwenye mtandao wa kijamii? Tafuta  
**#NorthantsTogether** kwa taarifa na ushauri  
kutoka NHS, Polisi, Halmashauri za Wilaya, na  
baraza la mitaa na mashirika mengine ya mitaa.

- Habari katika muundo na lugha zingine
- Ushauri wa kiafya
- Msaada kwa watu walio hatarini